

KIPEPERUSHI



KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KAHAMA (KEEC)



MEI, 2019

1. UTANGULIZI

Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kahama (KEEC) kilifunguliwa rasmi tarehe 18 Novemba, 2018 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Ufunguzi wa Kituo hiki ni matokeo ya utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Mhe Kassim M. Majaliwa kwa Baraza la Uwezeshaji baada ya jitihada za Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kutenga ardhi yenye ukubwa wa ekari 500 eneo la Zongomela katika Halmashauri ya Mji wa Kahama na kulipima viwanja na kuvigawa viwanja hivyo kwa Wajasiriamali. Kituo hiki kinaratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama. Kituo hiki kinahudumia wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na mikoa ya jirani.

2. MALENGO YA KEEC

Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kahama kimeanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha ama kuendeleza biashara na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kituo kinawakutanisha wadau mbalimbali wa uwezeshaji katika eneo moja ili waweze kutoa huduma kwa walengwa. Kituo hiki kinamrahisishia mwananchi kupata huduma za uwezeshaji katika eneo moja kwa mujibu wa malengo ya kituo kama yalivyoainishwa.

Kituo kinafanya mambo yafuatayo:-

- a) Kutoa huduma za elimu, ufundi stadi na ujuzi katika fani mbalimbali;
- b) Huduma za kurasimisha ardhi na biashara, upatikanaji wa leseni na vibali vyote vinavyohitajika katika biashara kama vile vibali vya shirika la viwango, mamlaka ya chakula na dawa, huduma za msimbomilia;
- c) Huduma za kifedha na mikopo;
- d) Elimu ya kodi;
- e) Elimu ya kuongeza thamani bidhaa;
- f) Huduma za mikopo nafuu ya serikali kutoka kwenye mifuko ya serikali,
- g) Huduma za bima ya afya;
- h) Huduma za hifadhi ya jamii,
- i) Elimu ya kuunda vikundi vya kiuchumi kama vile vyama vya ushirika nk
- j) Kituo kinatoa huduma za maeneo ya kufanyia aina mbalimbali za biashara kutokana na ukubwa wa eneo la kituo na mazingira husika;
- k) Huduma za masoko na kutengeneza mtandao wa masoko; na
- l) Ukumbi kwa ajili ya kuendesha mikutano.

3. WALENGWA WA KITUO

Walengwa wanaotarajiwa kunufaika na kituo ni wajasiriamali wote wakiwemo wadogo, wakati na wakubwa wakiwa mmoja mmoja, Vikundi ama Makampuni yaliyoko katika Sekta zote za kiuchumi na wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga na mikoa ya jirani.

4. TAASISI ZILIZOPO NDANI YA KITUO

Kituo cha Uwezeshaji kina taasisi 12 za uwezeshaji zinazofaya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa malengo ya Kituo yanatimia. Taasisi hizo ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), SELF Microfinance Fund (SELF MF), Asasi ya Kusaidia Sekta Binafsi za Kilimo (PASS Trust), Tanzania Chamber Of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), GSI Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Benki ya NBC Tanzania, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF); Huduma zinazotolewa na Taasisi hizo kwa wananchi zimeainishwa hapa chini:

a. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni mratibu wa Kituo hiki cha Uwezeshaji Kahama. Baraza ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Baraza lina dhamana ya kuhakikisha kuwa watanzania (wanawake, wanaume, vijana na watu wenye ulemavu) wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hapa nchini. Baraza linaratibu Programu mbalimbali za uwezeshaji kama vile Kijana Jiajiri, Kijana Jiandae Ajira, Programu ya Vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu, Programu ya Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, Programu ya Bodaboda nk.

b. Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)



Shirika la kuhudumia viwanda vidogo (SIDO) lilianzishwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge Na. 28 ya mwaka 1973 kupanga, kuratibu, kuendeleza na kutoa huduma mbalimbali kwa viwanda/biashara ndogo na za kati. Huduma hizo ni pamoja na Kutoa ushauri wa biashara, Mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali pamoja na masoko.



Walengwa wa SIDO ni Viwanda/biashara ndogo na kati, Wajasiriamali binafsi pamoja na vikundi vya Wajasiriamali chipukizi (wenye mawazo, wanaoanza na waliokwisha anza biashara), Mashirika/Taasisi zinazo saidia wajasiriamali, Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na jamii (NGOs)

c. SELF Microfinance Fund (SELF MF)

Mfuko wa SELF ulisajiliwa tarehe 04/09/2014 kwa Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002 chini ya Udhamini wa Serikali ili kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi hususan wa vijijini, na hivyo kuwapa fursa ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kujiongezea kipato ili kuondokana na umaskini. Huduma zinazotolewa na SELF MF ni pamoja na :



- i. Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo kupitia Asasi ndogo na za Kati za kifedha;
- ii. Kujenga uwezo wa Asasi Ndogo na za Kati kwa njia ya mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuwezesha Asasi hizi kujiendesha na kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi walengwa wa Mfuko; na

- iii. Kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji kwa tija, ikiwa ni pamoja na kuwekeza mikopo hiyo vizuri, na hatimaye waondokane na umasikini.

d. PASS TRUST



Ni chombo kilichoanzishwa Mwaka 2000 na kuanza utekelezaji kama mradi chini ya wizara ya Kilimo/Fedha ilikuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara na sekta zinazohusika.

PASS Trust inatoa huduma za maendeleo ya biashara kwa wateja kama Upembuzi yakinifu, Kuandaa Mipango ya Biashara, Kujenga utaalumu, Kuwaunganisha wakulima katika vikundi maalum kwa ajili yakilimo cha mkataba, kusambaza pembejeo kwa mkopo, kufanya mazungumzo ya bei na kutoa ushauri, na utafutaji na uunganishaji wa masoko PASS Trust pia inatoa huduma za fedhakwakuwasiadia watu na makampuni zinazostahili kupata mkopo kwa ajili ya uwekezaji wenye faida kupitia: Tahmini ya maandiko ya kuombea mkopo kulingana na masharti ya benki husika na kulinganishwa nabenkihizo: CRDB, NMB, NBC, AZANIA, EXIM, BOA, TIB, FBME, KCBL, TADB, AmanaBank, AKIBA COMMERCIAL BANK na TPB

Dhamana ya mkopo ambayo inatolewa kwa benki zenye mikataba ya kushirikianana PASS ili kujazia upungufu wa dhamana ya mteja



Walengwa wakuu wa Mfuko ni Mtu binafsi yeyote, vikundi, Chama au Kampuni zinazojishughulisha na sekta ya kilimo inaweza kutumia huduma za PASS, haswa:

- Wajasiriamali binafsi - ambao wanadira na wanyafanyabiashara katika hali ya ufanisi na kibiashara; na
- Wajasiriamali binafsi- watakaoshirikiana na PASS na Benki washirika na kuwakilisha nyaraka zinazo takiwa na ambao wanaweza kufikia angalau vigezo vya msingi kwa ajili ya ukopaji

Kipaumbele kitatolewa kwa wateja wenye matokeo makubwa katika mwendelezo wa mnyororo wathamani kwa bidhaa za kilimo hususani katika mazao ya chakula, biashara na mazao ya kusafirishwa nje ya nchi

e. Tanzania Chamber Of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA)



Ni Taasisi isiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa mwaka 1988, kwa lengo la kushirikiana na Serikali kuleta ufanisi katika sekta binafsi. TCCIA ni kiungo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Wajibu wa TCCIA ni kuandaa Mabaraza ya Biashara kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa, majadiliano, ushawishi na utetezi kwa Sekta binafsi (Dialogue, Advocacy & Lobbying), kutoa vyeti vya Uasili (Certificate of Origin), urasimishaji biashara, kutafuta ubia wa kibiashara, ushauri wa kibiashara, mafunzo ya ujasiriamali na VICOBA. kuandaa Maonyesho ya kibiashara na ziara za kibiashara.

Walengwa wa TCCIA ni Viwanda/Biashara ndogo na kati, Wajasiriamali binafsi, pamoja na vikundi vya Wajasiriamali chipukizi (wenye mawazo, wanaoanza na waliokwisha anza biashara), Mashirika/Taasisi zinazo saidia wajasiriamali, Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), wafanyabiashara wote, wakulima na wafugaji.

f. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)



Ni kati ya Programu za Serikali, zenye ofisi katika Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha Kahama. Lengo la Mpango huu katika kituo ni kuwawezesha wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara kushiriki katika uchumi rasmi unaosimamiwa na utawala wa sheria pamoja na Kujenga uwezo kwa watendaji wa Mamlaka za Serikali za mitaa kwa upande wa Tanzania Bara na wale wa Wizara za Kisekta kwa upande wa Zanzibar ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Urasimishaji Ardhi vijijini;
- ii. Urasimishaji Ardhi mijini;
- iii. Ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji;
- iv. Urasimishaji na uendelezaji Biashara;
- v. Kutoa mafunzo ili kuwawezesha wananchi kutumia Hati Miliki na Hati za Hakimiliki za Kimila katika kupata Mitaji kwenye Benki na Taasisi zingine za Fedha ili kuwaongezea kipato na kukuza uchumi.

Wananchi wa mijini na vijijini wanaomiliki rasilimali nje ya mfumo unaotambulika kisheria na wanaoendesha biashara bila kukidhi matakwa ya kisheria.

g. GSI Tanzania



Jukumu la GS1 ni kuwezesha biashara na kutoa msimbomilia. Kuanzia mwaka 2011, Tanzania imekuwa mwanachama wa GS1 ambayo ni taasisi ya kimataifa inayotoa msimbomilia (barcodes) na kutoa huduma ya ufatiliaji (traceability) wa bidhaa kutoka kwa mzalishaji hadi kufika kwa mlaji. Bidhaa zenye msimbomilia huongeza nafasi ya kupenya kwenye masoko ya ndani, kikanda na kimataifa, pia msimbomilia hurahisisha utambuzi wa bidhaa.



12345678

Kutokana na umuhimu wa msimbomilia kwenye kufanya biashara, wajasiriamali wote na wafanyabiashara wanashauriwa kusajili biashara zao na GS1 Tanzania ili kupata utambuzi wa bidhaa zao na cheti cha msimbomilia.

h. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)



Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.11 ya mwaka 1995, na ilianza kufanya kazi tarehe 1 Julai 1996. TRA ina jukumu la kusimamia kwa uadilifu kodi mbalimbali za Serikali Kuu. TRA inatoa huduma mbalimbali kwa wadau wake. Huduma hizi zinajumuisha: Usajili, Makadirio ya kodi, Ukaguzi wa Kodi, Kibali cha Forodha, Vibali na Leseni, Kujibu maswali na kushughulikia malalamiko, Kutoa nafuu ya kodi, Marejesho ya kodi, Huduma za uchunguzi wa masuala ya kodi, Elimu ya kodi, Utoaji wa data za kitakwimu na Mafunzo

i. BENKI YA NBC TANZANIA

Benki ya Taifa ya Biashara ni Benki ya zamani kuliko zote nchini Tanzania ikiwa na uzoefu wa zaidi ya miongo mitano. Benki hii inatoa huduma mbalimbali kwa wateja wa rejareja, biashara, mashirika na misaada ya uwekezaji, bidhaa na huduma za usimamizi mzuri wa fedha.

j. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)



VETA kwa kutumia Chuo cha ufundi stadi na huduma Shinyanga kinatoa mafunzo ya kozi za Elimu na mafunzo ya ufundi stadi ya muda

mrefu na mfupi kwa kutumia mfumo wa Umahiri (Competence Based Education and Training (CBET). Mfumo huu ambao hutumika duniani kote humfanya mwanafunzi kuwa mahiri katika fani anayojifunza.



Chuo kinauwezo wa kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi wapatao 400 kwa wakati mmoja katika fani kumi nazo ni Useremala, Ujenzi wa Nyumba, Ungaji Vyuma, Ushonaji, Ufundi Bomba, Uhazili na Kompyuta, Umeme wa Nyumbani, Ufundi Magari na Uendeshaji Mitambo (Plant Operation). Pia kina uwezo wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 430 wa kozi za muda fupi kwa wakati mmoja.

k. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)



Chuo kikuu huria cha Tanzania kilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 17 ya mwaka 1992 kuratibu, na kutoa elimu kwa njia ya huria, masafa na kimtandao. Mfumo wa utoaji elimu unamwezesha mwanafunzi kusoma huku pia akiwa anajishughulisha na shughuli zingine za kujipatia kipato.



Walengwa wa Chuo hiki ni wafanyakazi wa serikalini na taasisi binafsi, wahitimu wa elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita, wahitimu wa elimu ya ngazi ya cheti, stashahada, astashhada na shahada katika fani mbalimbali.

I. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF)



Mfuko wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo (The Agricultural Inputs Trust Fund) ulianzishwa mwaka wa 1994, kwa sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1994. na kufanyiwa marekebisho ya kwanza mwaka 2002. Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Pembejeo za kilimo ilikuwa ni utekelezaji wa Sera ya Serikali katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu. Hivyo, kazi ya Mfuko wa Pembejeo ni pamoja na :

- Kutoa mikopo ya riba nafuu ili kuwezesha kugharamia usambazaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na zana ndogondogo za kilimo;
- Kuhakikisha kuwa pembejeo zinawafikia wakulima na wafugaji kwa wakati na kwa bei nafuu
- Kutoa mikopo ya matrekta mapya matrekta madogo (*power tiller*) na kukarabati machakavu ili kuboresha na kupanua eneo la kilimo nchini.



Walengwa wa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo ni:-

- i. Wakulima au wafugaji kupitia kwenye vikundi,
- ii. Wakulima au wafugaji binafsi,
- iii. Vyama vya Msingi,
- iv. Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya,
- v. Vyama vya Akiba na Kukopa (SACCOS)
- vi. Mawakala wa kusambaza pembejeo,
- vii. Wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi

5. UTOAJI WA HUDUMA KATIKA KITUO

Kituo kinatoa huduma zake kwa kuzingatia Uwazi, Haki, Usikivu, Uwezo, Kuwajibika, Umoja na Kujituma. Kituo kinafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10: 00 Jioni ndani ya siku za kazi.

6. MATOKEO TARAJIWA YA KITUO

Kituo kinategemewa kusaidia kubadilisha hali ya uchumi kwa wajasiriamali katika mkoa wa Shinyanga na Mikoa ya Jirani, Aidha yafuatayo yanategemewa kutokana na matumizi ya huduma ndani ya Kituo.

- a. Kuongezeka kwa idadi ya Viwanda;
- b. Kuongezeka kwa ajira;
- c. Kuongezeka kwa pato la wananchi;
- d. Kupungua kwa kiwango cha umasikini;
- e. Kuongezeka kwa ajira;
- f. Kuongezeka kwa pato la Serikali;

- g. Kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi;
- h. Kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya fedha na elimu ya ujasiriamali;
- i. Upatikanaji wa Mitaji kwa wajasiriamali;
- j. Wananchi kupata fursa ya kushiriki katika masoko ya Ndani na Nje; na
- k. Kuongezeka kwa urasimishaji wa Ardhi na Biashara.

7. MAWASILIANO YA KITUO

- a) Mahali Kituo kilipo :
Barabara ya Tabora,
Kata ya Nyihogo
Halmashauri ya Mji wa Kahama
Mkoa wa Shinyanga
- b) Mawasiliano ya barua:
Meneja wa Kituo
Kituo cha Uwezesaji Wananchi cha Kahama
SLP 472
Kahama
- c) Mawasiliano ya barua pepe: nec@uwezesaji.go.tz
- d) Namba ya Simu : +255 22 2137362
- e) Tovuti : www.uwezesaji.go.tz